Mwananchi Alhamisi Julai 16, 2026 Pg 16

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

# Tanzania kurejesha hadhi ya reli ya Tazara

**Dar es Salaam.** Serikali imeahidi kuendelea kuimarisha miundombinu ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (Tazara) ili irejee kuwa mhimili muhimu wa uchumi, biashara na ujumuishaji wa kikanda, wakati reli hiyo ikiadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwake.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi, na Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, katika hafla ya chakula cha jioni ya kilele cha maadhimisho ya Jubilei ya Dhahabu ya Tazara iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema maboresho yanayofanywa yanalenga kuiwezesha reli hiyo kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye, huku ikiongeza mchango wake katika maendeleo ya Tanzania, Zambia na nchi za Kusini mwa Afrika.

Profesa Mbarawa alisema Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha reli hiyo inarejeshewa hadhi yake kama moja ya njia muhimu za usafirishaji barani Afrika.

Waziri huyo alisema ununuzi wa injini na mabehewa mapya, pamoja na matumizi ya teknolojia za kisasa, utasaidia kuirejesha Tazara miongoni mwa reli bora barani Afrika na kuimarisha nafasi yake ya kuunganisha Bandari ya Dar es Salaam na Zambia pamoja na nchi za Kusini mwa Afrika, hivyo kuchochea biashara na usafirishaji wa mizigo. Akizungumzia miaka 50 ya reli hiyo, Profesa Mbarawa alisema tukio hilo si sherehe ya reli pekee, bali ni kumbukizi ya mafanikio makubwa ya maendeleo katika historia ya Afrika yaliyotokana na maono ya viongozi waasisi, mshikamano wa kimataifa na urafiki wa Tanzania, Zambia na China.

Aliwataja Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa kwanza wa Zambia, Hayati Dk Kenneth Kaunda, na aliyekuwa Mwenyekiti wa China, hayati Mao Zedong, kuwa walioweka msingi wa mradi huo wakati wengi waliuona hauwezekani, na maono yao yakawezesha kujengwa kwa moja ya miradi mikubwa ya ushirikiano kati ya Afrika na China.

Kwa upande wake, Naibu Balozi wa Zambia nchini Tanzania, Anthony Bwalya, alisema Tazara ilikuwa njia muhimu ya kuifikia Bandari ya Dar es Salaam wakati wa harakati za ukombozi wa Kusini mwa Afrika na ilichangia kuimarisha uhuru wa kiuchumi wa Zambia.

Balozi wa China nchini Tanzania, Chen Mingjian, alisema China itaendelea kushirikiana na Tanzania na Zambia katika kuboresha miundombinu ya usafiri, kukuza biashara na kuhamasisha uwekezaji katika sekta za viwanda na kilimo.

Alisisitiza kuwa kuendeleza Tazara ni njia ya kuheshimu mchango wa wahandisi na wataalamu waliohusika katika ujenzi wa reli hiyo.

NIPASHE Alhamisi Julai 16, 2026 Pg 5

# Watu watatu wafariki dunia ajali ya malori yakigongana

**Na Mwandishi Wetu,**
**HANDENI** 0715086344
WhatsAPP SMS

WATU watatu wamefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa katika ajali ya barabarani inayohusisha malori mawili kugongana, katika barabara ya Handeni-Korogwe, eneo la Kata ya Sindeni, Tarafa ya Mzundu, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga.

Uchunguzi wa awali umebaini chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi, hivyo miongoni mwa hao waliofariki dunia ni madereva wawili magari hayo.

Ajali hiyo ilitokea usiku wa Julai 14, 2026, saa 4:30, ikihusisha gari lenye namba za usajili T 712 ABH, aina ya Mitsubishi Fuso, lililokuwa likitokea Handeni kuelekea Korogwe, na lingine lenye namba za usajili T 519 EMM, aina ya Eicher, lililokuwa likitokea Korogwe kuelekea Handeni.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Tanga Almachius Mchunguzi alisema,aliwataja waliofariki dunia ni dereva Yahaya Miraji (28), mkazi wa Handeni, na Japhary Ramadhan maarufu kwa jina la Ally (47), mkazi wa Tanga.

Mtu wa tatu aliyepoteza maisha ni mwanaume anayekadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 46 na 50 ambaye hadi sasa hajafahamika.

Aliwataja majeruhi ni Chenga Herbet (55) na Salama Ally (56), wote wakazi wa Muheza, ambao wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni.

Alisema Jeshi la Polisi limebaini kuwa chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi pamoja na uzembe wa madereva hao, hali iliyosababisha washindwe kuyamudu magari yao na hatimaye kugongana.

Miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni kwa ajili ya uchunguzi wa daktari pamoja na taratibu nyingine za kisheria.

Kamanda aliwataka madereva wote kuzingatia sheria za usalama barabarani, hususan kuepuka mwendo kasi, kuendesha kwa tahadhari na kuhakikisha wanazingatia alama zote za barabarani ili kupunguza ajali zinazoweza kuzuilika.

Alisema usalama barabarani ni jukumu la kila mtumiaji wa barabara, hivyo ushirikiano wa wananchi na uzingatiaji wa sheria ni muhimu katika kulinda maisha na mali za Watanzania.

CamScanner